22100297

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI A1 – HIGHER LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI A1 – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 1**
**SUAHILI A1 – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 1**

Thursday 13 May 2010 (afternoon)
Jeudi 13 mai 2010 (après-midi)
Jueves 13 de mayo de 2010 (tarde)

2 hours / 2 heures / 2 horas

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a commentary on one passage only.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N’ouvrez pas cette épreuve avant d’y être autorisé(e).
- Rédigez un commentaire sur un seul des passages.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario sobre un solo fragmento.


© International Baccalaureate Organization 2010

*Toa maoni yako juu ya* ***moja*** *ya tungo zifwatazo.*

**1.**

"Naam. Ala! Mbona hivyo? Si umemaliza shule. Ni lipi lililobaki kama si ndoa." Idi alimtania na kuacha tabasamu ling'arishe uso wake. Tumaini alichukuwa nafasi hiyo kumweleza mdogo wake kwani alishikilia kwa dhati mitazamo potovu kuhusu elimu ya wasichana. Alijua huu ndio wakati wa kumpa pwi na pwiriri ili ajinasue kutoka kwenye mawazo hayo ya kisenzi.

"Sikiliza kakangu nikueleze. Usijitie usogora kwa jambo usilolijua vizuri. Wazo kwamba msichana akimaliza shule hana lolote ila kuolewa, ni wazo la kale na lisilo na nafasi katika dunia ya leo. Msichana ana haki ya kuendelea na masomo, kadri ya uwezo wake. Kamwe jamii yake isimwekee mipaka na kuponza juhudi yake ya Kujiendeleza kwa lolote lile. Pingine hayo nisemayo ni kizungumkuti kwako, lakini utayaelewa siku moja." Tumaini alisita, kisha akaendelea, "Baba ameshikilia mawazo ya kizamani kwa dhati kiasi kwamba haoni umuhimu wa mimi kusoma zaidi. Idi, nikifaulu mtihani wangu, nitaenda chuo kikuu nisome zaidi hadi niwe daktari. Haya ndiyo matumaini yangu. Kwa hivyo, ondoa hizo fikra kongwe kuwa nataka kuolewa. Ndoa sio mwisho wa maendeleo ya mwanamke na usidhani nina mipango yoyote ya kuolewa na Sifa ati kwa kuwa ameniandikia barua. Hiyo siyo mara yake ya kwanza kufanya hivyo, na hakuna uchumba wowote hapa. Kwa hivyo, kaka mdogo, usiwazie jambo lisilokuwepo. Hilo ni mustahili kwangu," alikaulisha.

"Nimeelewa, lakini dada Tuma-kitambo umalize masomo ya chuo kikuu huoni utakuwa umepoteza muda mwingi na bahati yako ya kuolewa," kabla Idi hajaendelea, tumaini alimkatiza usemi na kumwambia, "Nani alikuambia ndoa ina mipaka ya umri? Ndoa haishurutishwi, wala hairidhishi ikiwa haitaamuliwa na wawili wapendanao. Ndoa ya kupangiwa na wazazi hairidhishi kwani kigezo cha mapenzi hakifikiriwi hapa. Ni vizuri iwapo wawili wapendanao watakuwa tayari kuoana kwa wakati ufaao kuoana. Sharuti za mila au wazazi huweza kuharibu maisha ya watu, na kumnyima nafasi kuyatambua yale ayatakayo maishani. Idi, usikubali kulazimishwa kuoa mapema ikiwa huko tayari. Utaishi maisha ya taabu kama akina Rehema," Idi alimsikiza dadake kwa maakini kisha akatamka.

"Usemayo yana maana, hasa katika ulimwengu wa sasa. Mimi nitasoma hadi pale nitakaposhindwa kutokana na uzee," alitania na kuachilia kicheko kilichopaa katika anga lile la magharibi.

"Naam, na siku za wanawake kuwategemea wanaume kwa kila kitu zimepita, lakini baba hataki kuukubali ukweli huu. Idi, usikubali kutekwa nyara na hoja muflisi za baba. Unaona jinsi alivyowaoza Rehema na Mashaka kwa tamaa ya mali? Usikubali kamwe Kuishi jana kama baba. Wewe ni kijana wa kisasa, kwa hivyo, ishi maisha ya kisasa." Tumaini aliendelea kumshauri.

"Mtazame Rehema, taabu anazopata zinatokana na maamuzi yake mwenyewe yaliyohimizwa na baba. Alikataa shule akaolewa. Mashaka naye alikataa kusoma hata baada ya kutafutiwa shule na Ba mdogo. Naye akaamua kuolewa. Baada ya muda, atakuwa mzigo kwa mumewe ambaye nasikia alifutwa kazi hivi majuzi."

"Ni kweli, sasa hushinda kutwa akitafuta vibarua mitaani kuyakimu maisha. Kazi ya kijungu jiko tu." Alitamka Idi.

"Kwa mashaka, hasa huo ni mwiba wa kujidunga, huambiwi pole. Aliyataka mwenyewe, sasa hana budi kuishi maisha ya taabu," aliongeza tumaini, kisha akatahadharisha, "yazingatie sana haya niliyokwambia Idi."

Idi aliashiria kukubali kwa kutikisa kichwa halafu aliagana na dadake na kwenda kwao. Tumaini alipokuwa akirudi alipitia kwa mzee Okwembo. Alimkuta amekaa mahali pake pa kila siku akichuuza dagaa.

"Mzee, leo hukupata wanunuzi au vipi? Mbona dagaa wanashindania nafasi ndani ya teo?" Tumaini alimuuliza baada ya salamu.

Clara Momanyi, *Tumaini* (2006)

**2.**

**Watu wa Mombasa**

Atani wa Kiwa-Ndeo, maneno mangi atani
musinene mupendao, yawatokayo kanwani
siku ya msu na ngao, na risasi matavuni
mtakwambiwa semani, la kunena msijue.

Simba kiwa mawindoni, hafunuwi zake ndole
huzivika mtangani, muinda asiziole
uliza utasakani, muinga uzingatile
nyoka za ng'ongo kobele, hatuchi situtisheni.

Hatuchi situtisheni, hatuituki mishindo
tangu kale na zamani, tuwazowevu wa kondo
ivu la moto wa kuni, tutalitenda kitendo
siku ya kutinda fumbo, tutaonana fundoni.

Kula mwenye mbovu niya, mwenye dhamirimbi nasi
rabi tatuhukumiya, tukuza zetu nafusi
kwa amri ya Jaliya, aliye Mola mkwasi
kufuata mfuwasi, hilo halipatikani.

Kula mwenye nia mbovu, kungwa mpindukiza 'ye
moka kiwana cha ivu, nale naaliyo naye
aifanyao mwelevu, mpe uyinga akaye
asikome mayutoye, afiliye mayutoni.

Kimbile mbele waume, zawakokota zisiki
taka nasi mutwandame, kwa khidima wa nyuki
pindani zisitwegeme, kwa miomo ya bunduki
tufiliye yetu haki, tusiwekwe cheo duni.

Mla shokowa la Pemba, na kwetu ataka kula
uyao kiwamba wamba, ili kwegesha madhila
meifanya kuwa simba, kuya pasi na sumila
ayapo takuya Shela, Suudi mutatendani?

Pani shauri Suudi, muniyuze na mapema
ambalo lenyi muradi, nanyi mu wana wazima
isiwe kutaradadi, iwapo siku ya kwima
tufe katika hishima, tusiwekwe cheo duni.

Na ndiya yenye kasidi, ni khasara kungiliwa
hishima yangu abadi, nda kurai na kwangowa
ni siraya ya biladi, ndipo mi kawatukuwa
hii mila ya wendiwa, yandesize tabasamu.

Na atiwe mwenye siri, musinegeshe shutuma
mi hila si kukithiri, nataka yenu salama
amali yangu ni kheri, kwepukana na malama
bisharaye na alama, humutowe kufahamu.

Shihabdin Chiraghdin, *Malenga wa karne moja* (1987)